# TAARIFA YA MAENDELEO YA HALMASHAURI YA MJI KIBAHA KWA MHESHIMIWA MHANDISI EVARIST W. NDIKILO MKUU WA MKOA WA PWANI KATIKA ZIARA YAKE TAREHE 24 OKTOBA, 2017

## 1.0. UTANGULIZI

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**, Halmashauri ya Mji Kibaha ni moja kati ya Halmashauri tisa za Mkoa. Ndani ya Halmashauri hii ndipo yalipo Makao Makuu. Kisheria Halmashauri hii imeanza kutekeleza shughuli zake rasmi mnamo mwaka 2004 baada ya kutangazwa rasmi na Waziri wa TAMISEMI (kwa sasa ofisi ya Rais – TAMISEMI) kupitia Gazeti la Serikali la tarehe 17/09/2004 G.N.352, kufuatia kusudio la Mheshimiwa Rais katika Gazeti la Serikali No.515 la mwaka 2002 ambalo halikupingwa.

Halmashauri ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba **750,** ambapo hekta **13,080** zinafaa kwa kilimo na zilizolimwa ni **6,932** sawa na asilimia **53**.

### Hali ya ulinzi na usalama.

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa**, Hali ya ulinzi na usalama katika Halmashauri yetu ni nzuri, hakuna tukio la uvunjifu wa amani lililo ripotiwa. Aidha wananchi wameendelea kutekeleza majukumu yao katika hali ya amani na utulivu.

## 2.0 WATUMISHI

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**, Ikama ya Halmashauri ya Mji Kibaha ni watumishi **1,693**. Waliopo ni watumishi **1,529** na upungufu ni watumishi **164**. Uhaba mkubwa wa watumishi upo katika Idara ya Utawala, Maji na Afya. Ili kukabiliana na upungufu huo Halmashauri inategemea kuajiri watumishi **73** ambao mishahara yao imetengwa na imeidhinishwa na Ofisi ya Rais -Utumishi na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

## 2.1 UHAKIKI WA WATUMISHI

Tangu kuanza kwa zoezi la uhakiki wa watumishi mwezi machi 2016, Halmashauri ilitekeleza zoezi kama ifuatavyo

### Uhakiki wa watumishi hewa,

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** uhakiki wa watumishi hewa ulianzia machi 2016 hadi Aprili 2017, jumla ya watumishi **20** waligundulika ni watumishi hewa na fedha zilizo okolewa ni shilingi **19,161,557.35**

**Uhakiki wa vyeti vya elimu.**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**, Zoezi la uhakiki wa vyeti vya Elimu ulifanyika kwa watumishi wote **1,539**, katika zoezi hilo watumishi **73** wameondolewa kwa kukutwa na vyeti vya kughushi, pia watumishi **8** waliondolewa kwa kukosa sifa za kidato cha nne wakati wana ajiriwa hivyo watumishi **81** waliondolewa kwenye mfumo wa malipo ya mshahara.

**Uhakiki uliofanywa na NIDA kwa kutumia mfumo wa Lowson**

Kati ya watumishi **1,529** wa Halmashauri ya Mji, Watumishi **1,438** walihakikiwa taarifa zao na watumishi **91** bado hawaja hakikikwa kwa sababu ya kutopata namba kutoka mamlaka ya vitambulisho NIDA.

**Mashauri ya nidhamu.**

**Mhe Mkuu wa Mkoa**, Jumla ya watumishi **28** wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa kufukuzwa kazi Kutokana na makosa ya utoro kazini, kughushi vyeti, na upotevu wa mali za Halmashauri. Kati yao Walimu **20**, Watendaji **3**, Tabibu **2**, Katibu Muhtasi **1**, Afisa Ardhi **1** na daktari **1**.

## 3.0 UKUSANYAJI WA MAPATO

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,** Mwak**a** 2016/2017 Halmashauri ilikadiria kukusanya shilingi **3, 954,400,000** katika vyanzo vya ndani na makusanyo halisi hadi kufikia 30 Juni, 2017 ilifanikiwa kukusanya shilingi **3,671,950,534**, sawa na asilimia **93**. Aidha mwaka 2017/2018 Halmashauri imekisia kukusanya shilingi **3,705,549,000** ambapo mapato halisi hadi Septemba 30, 2017 imekusanya shilingi **1,431,090,552** sawa na asilimia **38.6** ya makisio. Halmashauri ya Mji Kibaha imekua ya 1 katika ufungaji wa mahesabu ya serikali kwa mwaka 2014/2015 kati ya Halmashauri **186.**

## 3.1 SEKTA ZA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO

**Hali ya Uwekezaji wa Viwanda.**

**Mhe. Mkuu wa mkoa,** Halmashauri ya Mji Kibaha ina jumla ya viwanda **119** ambapo kati ya hivyo vikubwa **5**, vya kati **16** na vidogo **98**. Viwanda hivi vinafanya kazi. Aidha Kwa sasa kuna viwanda **4** Vinaendelea kujengwa ambapo vikukubwa **3** na vyakati **1**. Halmashauri imeendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji ambapo katika robo ya kwanza ya 2017/2018

imeweza kutumia shilingi **100,000,000** kufungua barabara eneo la Zegereni. Aidha Halamshauri imeendelea kupokea maombi ya wawekezaji mbalimbali na kuyafanyia kazi.

**Biashara na Masoko**

Halmashauri kupitia Sekta ya biashara imetoa leseni kwa wafanyabiashara rasmi **5,24**1 na zaidi ya wafanyabiashara **750** bado hawajarasimishwa. Aidha, Halmashauri inaendelea na taratibu za kuwarasimisha wafanyabiashara hao.

**Masoko**

Halmashauri ya Mji Kibaha ina soko la mnarani lenye vyumba **340** ambapo vyumba **200** vimekamilika na vyumba **140** bado havijakamilishwa na wamiliki ambapo vyumba **80** kati ya vilivyo kamilika wamefungua biashara zao. Aidha Paa la wauza nafaka lina wafanyabiashara **78,** paa la mama lishe lina wafanyabiashara **27**. Paa la wauzaji wa rejareja (ndani wenye meza kubwa **288**). Halmashauri imetoa namba '' **Cording"** katika vyumba vya sokoni tayari kwa kuanza kutoza kodi. pia imeweza kuhamisha wafanyabiashara waliokuwa wakifanya biashara eneo la mailimoja, na zoezi bado linaendelea.

## 4.0 HALI YA MAENDELEO YA KISEKTA

### 4.1 SEKTA YA ELIMU

**Elimu ya Awali**

Halmashauri ya Mji Kibaha ina shule/vituo vya awali **50** kati ya hivyo **39** ni vya serikali na **11** ni vya watu binafsi. Shule zote zina jumla ya watoto **3,834** kati yao wavulana ni **1,938** na wasichana ni **1,896.** Shule za serikali zina jumla ya watoto **3,300** ikiwa wavulana ni **1,685** na wasichana **1,615.**

**Elimu ya Msingi**

Halmashauri ya Mji Kibaha ina jumla ya shule za msingi **55** kati ya hizo **39** ni za serikali na **16** ni za binafsi zenye jumla ya wanafunzi **33,534**. Kati yao wavulana wapo **16,771** na wasichana **16,763**. Aidha kwa shule za Serikali kuna wanafunzi **29,052** kati yao wavulana **14,524** na wasichana ni **14,478**. Mwaka 2017 Halmashauri iliandikisha wanafunzi **4,800**

**Miundo mbinu Shule za Msingi za Serikali.**

Halmashauri inauhitaji wa vyumba vya madarasa **727** vyumba vilivyopo ni **301** na upungufu ni vyumba **426.** Pia Halmashauri ina uhitaji wa madawati

**8,584** yaliopo **8,714** na kuwa na ziada ya madawati **130.** Halmashaurii ina uhitaji wa matundu **1,294** ya vyoo yaliopo ni matundu **498** na pungufu ni **795.** Aidha Halmashauri inaupungufu wa majengo ya utawala **62** na upungufu wa nyumba za walimu **495.** Mwaka 2017/2018 Halmashauri imetenga shilingi **430,054,669** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu Msingi**.**

**Mitihani ya kumaliza elimu ya msingi na Ufaulu.**

Watahiniwa waliosajiliwa kufanya mitihani mwaka 2017 walikuwa **3,240** kati yao wavulana **1,631** na wasichana ni **1,609**. Waliofanya mitihani ni wanafunzi **3,234** kati yao wavulana **1,629** na wasichana ni **1,605** Aidha wanafunzi **6** hawakufanya mitihani kati yao wavulana **2** na wasichana **4** kutokana na sababu za utoro na ugonjwa. Aidha katika matokeo yaliyotangazwa mwezi Oktoba, Halmashauri ya Mji kibaha imekua ya kwanza katika Halmashauri 9 za Mkoa wa Pwani.

## 4.2 ELIMU YA SEKONDARI

Halmashauri ya Mji Kibaha ina jumla ya shule za sekondari **37**, kati ya hizo **13** ni za Serikali na **24** ni za binafsi. shule zote **37** zina jumla ya wanafunzi **10,992** kati yao wavulana ni **5,141** na wasichana **5,851**. Shule hizi zina jumla ya walimu **447**, na **15** ni watumishi wasio walimu. Aidha shule za Serikali zina jumla ya wanafunzi **7,216** kati yao wavulana **3,747** na wasichana **3,459.**

**Miundombinu Elimu Sekondari za Serikali.**

Halmashauri inauhitaji wa vyumba vya madarasa **205** vilivyopo ni vyumba **153** na upungufu ni vyumba **52**. Pia Halmashauri ina uhitaji wa madawati **7,206** yaliopo ni **6,657** na pungufu ni madawati **549**. Halmashauri pia ina uhitaji wa matundu **372** ya vyoo yaliyopo ni matundu **251** na pungufu ni **121**. Aidha, Halmashauri inauhitaji wa majengo ya utawala **13** yaliyopo ni **6** na upungufu ni **7**. Uhitaji wa nyumba za walimu ni **493** zilizopo ni **44** na upungufu ni nyumba **449** Halmashauri kwa mwaka 2017/2018 imepanga kutumia shilingi **520,000,000** kuongeza miundombinu ya elimu Sekondari

**Maandalizi ya mitihani ya kuhitimu kidato cha Nne na cha Pili.**
Mitihani ya kidato cha nne na cha pili inatarajiwa kufanyika tarehe 30/10/2017 ambapo watahiniwa wanaotarajiwa kufanya mitihani ya kidato cha pili ni **2,931** katika vituo **37** na watahiniwa wanaotarajia kufanya mitihani ya kidato cha nne ni **2,089** katika vituo **35** kati ya vituo hivyo vituo **34** ni watahiniwa wa shule na **1** ni kituo cha wanafunzi wa kujitegemea.

## 4.3 SEKTA YA MAJI

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**, Vyanzo vikuu vya maji katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha ni bomba la DAWASCO, visima virefu **2** na lambo **1** ambavyo vinahudumia wakazi **73,771** sawa na asilimia **57**. Aidha Kupitia programu ya maji na usafi wa mazingira, Halmashauri ilipanga kutekeleza miradi **11** katika mitaa **15** ambapo mpaka sasa miradi **6** imekamilika, miradi **5** inaendelea na ujenzi ambapo imefikia wastani wa asilimia **84** katika hatua za utekelezaji. Halmashauri Mwaka 2016/2017 ilipokea shilingi **390, 402,933** kutoka Serikali kuu kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo kwa mwaka huu 2017/2018 imepangwa kutumia shilingi **124, 324,000/=** ili kuendeleza ujenzi wa miradi ya maji.

## 4.4 SEKTA YA MIFUGO

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Idara ya Mifugo, uvuvi na umwagiliaji katika kipindi cha 2016/2017 imeendelea kutoa elimu za ufugaji bora kwa wafugaji **403**, matumizi ya teknolojia ya uhamilishaji ili kuwa na koo bora za mifugo kwa wafugaji **127** ambapo Jumla ya ng'ombe **271** walipandishwa. Halmashauri pia imetoa dhamana kwa vikundi **2** vya wafugaji wa sungura katika Kata ya Pangani. Aidha imeendelea kuhamasisha ufugaji wa samaki ambapo mabwawa ya samaki **72** yamechimbwa kati ya hayo **69** yamepandwa samaki. Jumla ya tani **11.3** zilizalishwa kwa mwaka 2016/2017**.**

**4.5 SEKTA YA KILIMO NA USHIRIKA.**

Halmashauri ya Mji Kibaha ina Hekta **13,080** zinazofaa kwa Kilimo ambapo hekta zilizolimwa ni **6,932**. Jumla ya wakulima katika Halmashauri ni **11,479**.

**Hali ya chakula**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Mahitaji ya chakula kwa Halmashauri ya mji kwa mwaka ni **tani 28,138** za wanga **tani 11,721** za utomwili. Hali ya upatikanaji wa chakula ni ya utoshelevu. Wananchi wanapata vyakula kutokana na mavuno ya msimu uliopita ambapo tulivuna Jumla ya **tani 2,698** za wanga na **tani 57** za Utomwili.

Aidha wananchi wengi wanaendelea kupata vyakula vinavyopatikana katika maduka na masoko yetu kwa bei ya kuridhisha ambapo bei za vyakula zimeendelea kushuka ukilinganisha na mwaka uliopita (Mfano unga wa mahindi umeshuka toka sh. **1,500** kwa kilo mwezi Septemba 2016 hadi wastani wa sh**. 1000** mwezi Oktoba 2017).

Wilaya imejiwekea mikakati mbalimbali ya kukabiliana na upungufu wa chakula ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wakulima kuandaa mashamba mapema kipindi hiki cha vuli ambapo kila kaya ya mkulima imehimizwa kuwa na Ekari moja ya Muhogo na ekari moja ya zao la biashara. Aidha uboreshaji wa Masoko ya vyakula unaendelea ili wasiojishughulisha na kilimo wapate vyakula kupitia masoko haya.

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,** Elimu kwa wakulima kuhusu kilimo bora cha mazao ya chakula na biashara imeendelea kutolewa kupitia mashamba darasa ambapo Jumla ya wakulima **2,475** wamezalisha miche **21,000** ya mikorosho ukilinganisha na miche **4000** kwa msimu wa 2015/2016. Aidha zoezi la upuliziaji mikorosho linaendelea na jumla ya wakulima **415** wametumia madawa ya ukungu na wadudu na kuwezesha jumla ya miti **27,200** ya mikorosho sawa na Hekta **388** kupuliziwa. Makadirio ya mavuno ni tan**i 405** za korosho msimu wa 2017/2018 ukilinganisha na malengo tani **394** zilizozalishwa mwaka 2016/2017. Aidha Kutokana na kutoa elimu ya stakabadhi mazao ghalani msimu wa 2016/2017 tulikusanya Jumla ya tani **906** katika maghala **2** yaliyo teuliwa.

**Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo:**

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,** Jumla ya **tani 27,200** za madawa ya korosho kwa mfumo wa ruzuku zimesambazwa kwa wakulima **415** katika **kata 10** zinazolima korosho. Aidha pembejeo nyingine kama Mbolea za kupandia na kukuzia zinapatikana madukani na wasambazaji wameelekezwa kufuata bei Dira ya **sh. 49,295** na **36,716** kwa mfuko wa **kilo 50** wa mbolea ya DAP na UREA katika eneo letu la Mji Kibaha.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Maandalizi ya Mfumo wa stakabadhi ghalani unaendelea ambapo maghala **2** ya Kongowe na Misugusugu yeme pendekezwa kutumika kama kituo cha ukusanyaji wa korosho kabla ya korosho kupelekwa katika ghala la mnada litakalopendekezwa na Bodi ya Korosho kwa msimu huu. Wakulima wanaendelea kuelimishwa kuokota na kukausha korosho wakisubiri Mnada na pia kuwapa elimu kuhusu maandalizi ya mvua za vuli kwa kuandaa mashamba yao mapema na kupanda mazao ya muda mfupi na yanayostahimili ukame kama Mihogo,Mahindi, Viazi vitamu, Mtama na Jamii ya Mikunde.

## 4.6 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

**Mhe. Mkuu wa Mkoa** Halmashauri katika kipindi cha 2016/2017 ilipanga kutoa mikopo kwa wanawake na vijana shilingi **391,100,000** ambapo hadi kufikia 30 Juni Halmashauri iliweza kuchangia shilingi **174,000,000** katika vikundi **96** vya wajasiliamali na vijana. Aidha, Mwaka 2017/2018 Halmashauri imechangia shilingi **70,000,000** katika mfuko wa wanawake na vijana. Halmashauri imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli zinazofanywa na sekta binafsi zinazohusu watu wenye uhitaji maalum.

## 4.7 UJENZI NA MIUNDOMBINU

Idara ya ujenzi katika kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi kufikia sasa inaendelea kutekeleza na kusimamia miradi mbalimbali ya Halmashauri,
Miradi hiyo ni Ujenzi wa kituo cha Mabasi (Kibaha Bus stand) kinachojengwa eneo la CBD, Ujenzi wa barabara za lami eneo la CBD na Mkoani zenye urefu wa km **3.62**. Miradi hii inatekelezwa kwa ufadhili wa fedha kutoka Benki ya Dunia.

Vilevile Halmashauri ipo kwenye maandalizi ya ujenzi wa Soko la kisasa eneo la CBD ambapo Halmashauri inatarajia kukopa fedha benki ya TIB. Hata hivyo

Kutokana na wafanyabiashara kuhamishiwa eneo la Mnarani, kazi inayofanyika kwa sasa ni"Design Review" ya Soko la kisasa ambapo Mhandisi Mshauri alipewa dondoo za rejea za kufanya kazi hiyo ambayo anaendelea nayo ili ujenzi uanze kutekelezwa.

Halmashauri inaendelea pia kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi za Makao Makuu, kazi zinazofanyika kwa sasa ni kumwaga nguzo, (beam) na kupaua, kazi hiyo inafanywa na mkandarasi SUMA JKT akisimamiwa na Mhandisi mshauri Chuo kikuu cha Ardhi. Aidha Maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Soko la Mnarani – NIDA kwa kiwango cha lami yanaendelea, kwa sasa yapo kwenye hatua za manunuzi.

**Mh Mkuu wa Mkoa**, Idara inaendelea kutoa vibali vya ujenzi na kutoa elimu kwa wananchi kupitia kwa Watendaji wa kata kuhusu taratibu za ujenzi ili taratibu ziweze kufatwa

## 4.8 SEKTA YA ARDHI, MALIASILI NA MIPANGOMIJI

**Mhe. Mkuu wa Mkoa** Halmashauri kwa mwaka 2016/2017 imefanikiwa kukamilisha uandaaji wa mpango kabambe ( Master Plan 2014 - 2034) na kuiwasilisha Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya makazi kwa hatua ya ukamilishaji na kuwa mpango kamili. Aidha Halmashauri imepima viwanja **1,936** katika maeneo mbalimbali na kuyatambua mashamba pori **4** na kuweza kuwapa ilani ya kuyafuta. Pia imebuni michoro wa Mpango miji wenye Jumla ya viwanja **932** katika eneo lililokuwa shamba la Wizara ya kilimo na Mifugo (MITAMBA) ambapo Jumla ya viwanja **500** vimepimwa. Katika eneo la Zegereni Michoro **3** imeandaliwa yenye viwanja **167** na viwanja **70** vimepimwa.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa** , Halmashuri inampango wa kurasimisha makazi ya mitaa ya Mailimoja, Uyaoni na Tangini kikao cha kwanza na wananchi hao tayari kimefanyika na kuwa na hoja endapo eneo la mita **60** litaongezwa kuvunjwa ambapo Halmashauri imeshindwa kutoa majibu ya moja kwa moja na kuwaahidi wananchi kuwa wataalikwa kwakala wa barabara Mkoa wa Pwani (TANROAD) ili kutoa ufafanuzi.

## 4.9 SEKTA YA USAFI NA MAZINGIRA

Sekta ya usafi na mazingira kwa mwaka 2016/2017 iliweza kukusanya taka tani **30.489**, pia Halmashauri imezika maiti **14** ambao wasio kuwa na ndugu. Aidha halmashauri imeendelea kusafisha Mji na kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzaniala kufanya usafi kila jumamosi ya mwisho ya mwezi

## 4.10. SEKTA YA AFYA.

**Mhe. Mkuu wa mkoa** Halmashauri ya Mji Kibaha ina jumla ya vituo **36** kati ya hivyo **12** ni vya Halmashauri na **24** ni vya watu binafsi, jeshi na mashirika ya dini. Kati ya hivyo vituo vya Afya ni **6** zahanati **30** clinic na maabara pekee binafsi **5.**

### Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** upatikanaji wa dawa na vifaa tiba unaendelea kuimarika katika vituo vyetu. Mwaka 2016/2017 dawa na vifaa tiba toka ruzuku ya Serikali kuu zilipokelewa kiasi cha shilingi **93, 799,180,000** sawa na ongezeko la asilimia **30** ukilinganisha na mwaka 2015/2016. Aidha kwa mwaka 2017/2018 Halmashauri imepokea dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi **29, 543,300/=.**

### Mapambano dhidi ya Malaria.

**Mh. Mkuu wa Mkoa,** Utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Halmashauri ilipokea dawa ya Viuadudu madumu **26** yenye ujazo wa lita **20** ikiwa ni jumla ya lita **520** yenye thamani ya shilingi **6,864,000**. Zoezi la unyunyiziaji dawa umetekelezwa kwa kata **5** ambazo zina jumla ya mazalia **763** ambapo mabwawa ya kudumu ni **16**, mazalia ya muda **55,** madimbwi **155** na mazalia ya ndani **537.** Dawa hizi zimenyunyizwa katika Kata za Tangini, Mkuza, Picha ya ndege, Tumbi na Maili moja

### Taarifa ya utekelezaji wa matokeo makubwa sasa ( BRN na RBF)

**Mh. Mkuu wa Mkoa**,Wizara ya Afya imefanya tathmini katika zahanati. Katika tathmini hiyo zahanati **10** zilipata nyota **3,** zahanati **5** zilipata nyota **2**, zahanati **11** zilipata nyota **1** na zahanati **2** zilipata nyota **0**. Vituo vya Afya **3** vilipata nyota **3** na zaidi, kimoja kilipata nyota **2** na **2** vilipata nyota **1**.

Aidha kati ya vituo **12** vya Halmashauri , Vituo **11** vilipata nyota **3,** kituo **1** kilipata nyota **2.**

**Mradi wa Malipo kwa ufanisi ( RBF)**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Halmashauri imepokea fedha za RBF "sart up fund" kiasi cha shilingi **120,000,000** kwa vituo **12** vya Halmashauri ya Mji. Fedha hizi zimetumika katika kukarabati na kujenga vichomea taka, shimo la kutupia kondo la nyuma, kuzungushiwa uzio na kujenga vyoo bora.

Vituo **7** viliingizwa kwenye mradi wa awamu ya kwanza kwa kuwa vituo **5** havikuwa na sifa (Nyota). Katika awamu ya nne vituo vyote **12** vya Halmashauri vimeingia katika mradi na tayari vimefanyiwa tathmini iliyokamilika tarehe 20 Oktoba, 2017. Katika ulipaji wa malipo kwa ufanisi umefanyika kwa robo tatu ambao shilingi **147,679,138.32** zimetolewa

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KITAIFA

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Halmashauri imeendelea kusimamia na kutekeleza maagizo ya kitaifa kama ifuatavyo.

### a. Kutenga asilimia 60 ya mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Katika kutekeleza agizo hili Halmashauri ya Mji Kibaha kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitenga shilingi **2,390,000,000** za mapato ya ndani ikiwa ni asilimia **60** katika shughuli za maendeleo ambapo hadi kufikia 30 Juni Halmashauri ilichangia shilingi **1,699,497,490** sawa na asilimia **71** katika miradi ya maendeleo. Mwaka 2017/2018 Halmashauri imetenga shilingi **2,238,309,406** ikiwa ni asilimia 60 ya mapato ya ndani katika shughuli za maendeleo, hadi kufikia 30 Septemba Halmashauri imechangia shilingi **906, 000,000** sawa na asilimia **40**.

### b. Ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za kielekroniki.

**Mhe.Mkuu wa Mkoa,** Halmashauri imefanikiwa kukusanya mapato kwa kutumia mashine za kielektroniki katika vyanzo vyake vya mapato kama ilivyo elekezwa.

**c. Kufanya usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Halmashauri imeendelea kusimamia zoezi la ufanyaji wa usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi ambapo kila Kata inatekeleza agizo hilo la kuwataka wananchi wote kufanya usafi katika maeneo yao ya makazi na biashara na wasiofanya usafi kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za mazingira na Afya.

**d. Kufanya mazoezi kila Jumamosi ya pili ya Mwezi**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Katika kutekeleza agizo hili Halmashauri imeendelea kuwahamasisha wananchi wa Mji wa Kibaha na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali kufanya mazoezi kila mwezi. Wananchi wameendelea kuhamasika na kujitokeza, kwa mwezi Oktoba Taasisi za magereza, Polisi, jeshi la zimamoto Njuweni hoteli, watumishi wa Halmashauri ya Mji Kibaha, Shule ya Sekondari Bundikani, Mwanalugali na Shule ya msingi mamlaka, mailimoja na maendeleo walijitokeza kufanya mazoezi.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa** kila mwezi unakaulimbiu yake ambapo mwezi Oktoba ilikuwa na kauli mbiu isemayo **"hakika mazoezi ni tiba isiyo na gharama**" ambapo mgeni rasimi alikua ASP Mkuu wa kikosi cha FFU Mkoa wa Pwani. Aidha kila mwezi kunamshindi (kwa mpira wa miguu) katika mwezi huu mshindi alikua ni Jeshi la Magereza dhidi ya UJOKI (UMOJA WA JORGING KIBAHA)

**e. Kuondoa wavamizi ndani ya msitu wa hifadhi Ruvu kazkazini**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Oparation ya kuwaondoa wavamizi ndani ya msitu wa hifadhi ya Ruvu imefanyika tarehe 12/10/2017 hadi 17/10/2017 ambapo jumla ya mifugo **877** ilikamatwa kwa machanganuo ufuatao. Ng'ombe **814** , mbuzi **45**, kondoo **17** na punda **1**. Aidha jumla ya shilingi **14,300,000** ziliweza kukusanywa kama maduhuli wakati wa doria maalum. Pia mifugo iliokuwa ndani na pembezoni mwa hifadhi iliweza kuondolewa, vilevile vibanda na wavamizi wenye makazi na wakulima waliondolewa na kuwafunguliwa mashtaka **RB. Bag/3007/2017**

## 6.0 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA MHE. MKUU WA MKOA KATIKA SHUGHULI ZA MAENDELEO ALIYOYATOA MWEZI AGOSTI, 2017

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Utekelezaji wa maagizo yako uliyo yatoa mwezi Augosti 2017 ni kama ifuatavyo.

1. **Kuanza kukusanya kodi ya maduka yaliyopo Soko la Mnarani**.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**. Katika kutekeleza agizo hili tathmini imefanyika, orodha ya maduka imeandaliwa na ina jumla ya vyumba **340** ambapo vyumba **200** vimekamilika, na vyumba **140** bado havijakamilika. Aidha, Halmashauri imetoa namba katika vyumba **340** tayari kwa kuanza kulipia Kodi ifikapo Novemba, 2017.

2. **Eneo la Wafanyabiashara ndogondogo lisawazishwe**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**. Katika kutekeleza agizo hili eneo la Wafanyabiashara ndogondogo, limesawazishwa na kazi ya kuweka kifusi na kukisambaza imekamilika.

3. **Upatikanaji wa huduma ya maji kwenye vyoo**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**. Taratibu za malipo zimeshafanyika na DAWASCO tayari wamepeleka maji katika vyoo vipya vya soko.

4. **Wafanyabiashara wa Mailimoja wenye maeneo soko la Mnarani wasipatiwe leseni**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**, Katika kutekeleza agizo hili wafanyabiashara wa Mailimoja wenye vyumba soko la mnarani hawajahuishiwa leseni zao mpaka pale watakapo hamia soko la mnarani.

5. **Kuwepo na mikataba ya upangishaji vibanda soko la Mnarani**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**, Halmashauri kwa kumtumia mwanasheria wake imeandaa mikataba ya kupangisha vibanda katika soko la Mnarani na mikataba iko tayari kwa kusainiwa.

6. **Kuzuia biashara katika stendi ya Mailimoja**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**, Katika kutekeleza agizo hili Halmashauri imewaondoa wafanyabiashara wote katika eneo la stendi ya Mailimoja na kuweka doria ya mgambo ambao wanahakikisha wafanyabiashara hawarudi eneo hilo. Zoezi ni endelevu

7. **Miundombinu ya taa iboreshwe, taa ziongezwe**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**, Agizo limetekelezwa Halmashauri imeweka miundombinu ya taa katika eneo la Mnarani na tayari zinawaka.

**8. Kuwepo kwa kituo cha Polisi sokoni.**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,** Katika kutekeleza agizo hili eneo la kujenga kituo cha polisi limetengwa, ambapo mchoro wa Ofisi ya Polisi umeandaliwa, mchanganuo wa gharama za jengo zima litakalohusisha Ofisi za wakusanya ushuru wa standi ndogo unaandaliwa.

## 7.0 HITIMISHO

**Mhe. Mkuu wa Mkoa.** Dhamira ya Halmashauri kwa 2016-2021 ni Kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu na kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya kuwekeza kwa matumizi mazuri ya rasilimali zilizopo kwa maendeleo endelevu. Tunaendelea kuhakikisha kuwa dhamira hii inatekelezeka hasa kwa kubaini fursa za kiuchumi zilizopo, kuongeza mapato na kuzifanyia kazi kama tulivyo ainisha hapo juu.

**Naomba kuwasilisha.**

**Assumpter Nshunju Mshama**
**MKUU WA WILAYA**
**KIBAHA**